26 Mei 2015

TATHMINI YA 17 YA LDGI KUHUSU ARDHI

MABADILIKO YA SEKTA YA ARDHI BAADA YA UTEKELEZWAJI KWA MIAKA MITANO

Utangulizi

Kufuatia kupitishwa kwa katiba mpya tarehe 27 Agosti 2010, nchi hii ilirejelea kuangazia mabadiliko muhimu ya kisheria na kitaasisi ilivyoratibiwa kwenye sura ya tano inayohusu Ardhi na Mazingira. Kipengee cha tano kinatoa mwelekeo wa kiwakati kwa utekelezwaji wa sheria. Muda uliotengewa kila sehemu ya vipengee vya kisheria ulianza siku hiyo hiyo ilipoidhinishwa katiba. Mwezi Desemba mwaka 2009 Kenya ilikuwa imejipatia Sera ya Ardhi ambapo falsafa zake zilitoa mwongozo kwa yaliyomo kwenye sura inayohusu Ardhi na Mazingira katika katiba.

Huku sera ya ardhi pamoja na katiba zikitoa fursa za nia, ni sheria maalum inayowezesha utekelezwaji wa vipengee kadha wa kadha vinavyotoa mwelekeo kwa sera fulani na nia ya kikatiba. Ni jambo la busara basi kwamba sheria inayoundwa itilie maani sera pamoja na matarajio ya kikatiba ya wakenya. Bila kusahau, kunapojiri hali kama humu nchini ambapo kuna sera hali kadhalika katiba, ili kuepuka mkwaruzano, katiba itazingatiwa na itatumika kufafanua sheria. Ni dhahiri kuwa kila mojawepo wa sheria za ardhi zinazotekelezwa kwa sasa inatoa nafasi kwa kubuni sheria kabambe zitakazofafanua shughuli, utaratibu pamoja na yaliyomo. Aidha haya hayajatekelezwa. Basi bila sheria kama hizo, utekelezwaji utakuwa wa mapendeleo na hivyo kuathiri shughuli nzima.

Aghalabu, kasoro na migogoro ya kisheria hujitokeza isivyofaa wakati wa utekelezaji. Hili linaweza kuzua mizozo, kuzembea, kucheleweshwa au hata utekelezaji isivyofaa. Kenya iko katika shughuli ya kuandikisha changamoto haswa inapofikia utekelezaji. Ile bayana inayoendelea kujitokeza ni kusitisha shughuli kwa Wizara ya Ardhi ambayo ilikuwa inatoa na kusimamia ardhi ya umma, pamoja na Tume ya Ardhi iliyoundwa majuzi inayosimamia ardhi ya umma kwa niaba ya serikali kuu na zile za kaunti. Pia kumeshuhudiwa ukosefu wa uhakika pamoja na kucheleweshwa kwa shughuli. Hata hivyo haya ni wazi kabisa. Ukaguzi dhabiti wa

utekelezaji unaweza kutoa fursa kwa habari kamili. Inapaniwa kuwa shughuli za kisheria zijazo zitatoa mwongozo wa kutatua mizozo na changamoto zote kwa kufanya marekebisho ya kina kwa sheria iliyoko. Aidha inatarajiwa kuwa bunge litafanya hala hala kuidhinisha sheria hizo za ardhi.

I. Hatua zilizopigwa kuwezesha shughuli za kisheria

Zifuatazo ni sheria zilizopitishwa chini ya miaka 5:-

1. Sheria ya Mazingira na Mahakama ya Ardhi, 2011 (*Inatoa mwongozo wa kutatua mizozo*)
2. Sheria ya Ardhi, 2012 (*Inafafanua haki, majukumu na shughuli kwenye ardhi ya umma na kibinafsi*)
3. Sheria ya Usajili wa Ardhi, 2012 (*Inaelezea shughuli za usajili wa hati miliki za ardhi*)
4. Sheria kuhusu Tume ya Kitaifa ya Ardhi, 2012 (*Inafafanua majukumu ya Tume ya Kitaifa ya Ardhi*)
5. Sheria kuhusu Mali iliyopatikana kwa Ndoa, 2013 (*Hufafanua haki na majukumu ya waliooana kwa kuzingatia mali iliyochumwa*)

Sheria zinazofaa kuhakiki muda uliotolewa kikatiba na zilizo lazima zipitishwe kuwa sheria kwa chini ya muda wa miezi 3 ijayo la sivyo bunge liwe limevunja katiba ni zifuatazo:-

1. Mswada kuhusu Ardhi ya Jumuiya, 2014 (Ibara 63)
2. Mswada wa Maridhiano kuhusu Raslimali (Kufanyiwa marekebisho na bunge), 2015 (Ibara 71)
3. Mswada wa Uchimbaji Madini, 2014 (Ibara 71)
4. Mswada wa Mpangilio wa Ramani ya Ujenzi 2014 (Ibara 66)

Nyinginezo zinazokaribiana japo hazijapitishwa ni:-

1. Mswada wa Kawi, 2015
2. Mswada wa Petroli (Uvumbuzi, Ukuzaji na Uzalishaji), 2015
3. Mswada wa Raslimali, 2014
4. Mswada wa Ufurushaji na Makazi, 2014
5. Mswada wa Kuzuia na Kudhibiti Uchafuzi wa Maji, 2014

Ifahamike kuwa marekebisho ya sheria za utumizi wa ardhi zinazohitaji sheria zilizoko kupangwa kikamilifu ilivyoratibiwa kwenye Ibara 68(b) yanasubiriwa. Hili lilitarajiwa ifikapo

mwezi Machi 2015 kwa kuwa Tume husika iliingia mamlakani mwishoni mwa mwezi Februari 2013.

II. Hatua zilizopigwa kwa mipango ya sekta husika

Baadhi ya mipangilio ya kisekta, japo imetekelezwa kiholela kwa muda wa miaka mitano iliyopita, inazingatia mapendekezo na misingi ya sera ya ardhi pamoja na katiba. Hii ni kama ifuatavyo:-

- Kubuniwa kwa Mahakama ya Mazingira na Ardhi ili kutatua mizozo husika nchini kote ilivyoratibiwa kwenye irabu za 162 (2) (b) na 60 (1)(g) ya katiba.
- Baadhi ya viungo vya kiteknolojia kama usajili kidijitali, kupiga uyoka rekodi za ardhi pamoja na kutoa kodi za ardhi bila kusaza shughuli za kusaka, yote haya yakipania kukuza uwazi na urahisi kwenye shughuli ya usimamizi wa ardhi inavyodokeza Ibara 60 (1)(d). Wa aidha, ukaguzi pamoja na upangaji faili unaoendelea kwenye sajili za ardhi chini ya wizara ya Ardhi ni mambo yanayokubalika.
- Mipango ya kutoa Hati miliki na kuchora ramani ilivyoratibiwa kwenye ibara 60 (1)(c), imeelekezwa baadhi ya maeneo ya Pwani, Mashariki na Bonde la Ufa. Kituo cha kutekeleza shughuli hiyo muhimu tayari kimezinduliwa.
- Tume ya Ardhi kurejesha ardhi iliyopokezwa kinyume cha sheria ili kuafikiana na Ibara 67 (2)(a) na 68 (c)(v). Hili lilifanyika kwenye maeneo ya kaunti ya Lamu na linaendelea kutekelezwa kwa utoaji wa ardhi kwenye maeneo ya miji nchini japokuwa macho yote yameelekezewa Kaunti ya Nairobi.

III. Mapendekezo

Taasisi ya Usimamizi na Maendeleo ya Ardhi inapendekeza:-

1. Kuwa bunge (La Kitaifa na lile la Senate) kujizatiti ili kukamilisha mswada ulio pembeni wa Ardhi ya Jumuiya, Maridhiano kuhusu Raslimali (Kufanyiwa marekebisho na bunge), Mswada wa Uchimbaji Madini na Mswada wa Mpangilio wa Ramani ya Ujenzi ambayo yote inafaa kuhakiki muda uliotolewa kikatiba wa miaka mitano inayotamatika tarehe 27/08/2015, miezi mitatu kutoka sasa.
2. Kuwa bunge lipitishe udhibiti kwa sheria ya Ardhi, Usajili wa Ardhi pamona na ile ya Tume ya Kitaifa ya Ardhi, zote zinazotumiwa licha ya ukosefu wa mwelekeo kabambe.

3. Kuwa bunge liidhinishe mapendekezo yatakayoziba nyufa na uwezekano wa mizozo inayojitokeza kwenye sheria ya Ardhi, Sheria ya Usajili wa Ardhi pamoja na Sheria ya Tume ya Ardhi ili kuondoa vipengee vinavyozua utata.
4. Kuwa bunge lisaidie wizara husika pamoja na Tume ya Kitaifa kuhusu Ardhi kuharakisha utengenezaji wa sheria zinazokaribiana tayari kwa utekelezwaji.
5. Kuwa Wizara ya Ardhi pamoja na Tume ya Ardhi kubuni ramani ya ushirikiano inayotangamana na mabadiliko ya ardhi ili mipango yote itakayotekelezwa na mojawepo wa taasisi hizo inaweza kuimarishwa kwa shughuli za mipango inayoendelezwa na wale wanaofaa kutekeleza, wanaofaa kukadiria bajeti, washikadau bila kusahau bunge.

Imetolewa na Taasisi ya Usimamizi na Maendeleo ya Ardhi tarehe 26 Mei 2015